

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

MREJESHO WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Halmashauri ilikuwa katika maandalizi ya kukamilisha rasimu ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2021/2022. Baada ya kujadiliwa na kupitishwa katika vikao mbalimbali ngazi ya Halmashauri na Mkoa kwa mujibu wa kanuni na taratibu, rasimu hiyo iliwasilishwa Hazina kwa ajili ya majadiliano. Pia, kwa nyakati tofauti iliwasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI na Kamati ya Bunge kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maelekezo. Aidha, Rasimu iliwasilishwa Bungeni, ikajadiliwa na kupitishwa.

Katika vikao vya kupitisha Rasimu ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri vilivyofanyika mwezi Disemba 2020 hadi Januari 2021 vilipitisha makisio ya mapato na matumizi ya kiasi cha Shilingi **Sh 46,512,442,772.00** kama inavyoonesha katika jedwali.

A) MAPATO

Na	Chanzo cha mapato	Kiasi
1	Serikali Kuu	37,152,001,000.42
2	Mapato ya ndani	5,306,258,756.00
3	Wahisani	4,054,183,015.58
JUMLA		46,512,442,772

B) MATUMIZI

Na	Aina ya Matumizi	Kiasi
1	Mishahara	32,831,658,000.00
2	Matumizi ya kawaida	5,388,061,036.00
3	Miradi ya maendeleo	8,292,723,736.00
JUMLA		46,512,442,772.00

Kutokana na maelekezo kutoka mamlaka husika, kuna mabadiliko yaliyojitokeza katika viwango vya ukomo wa bajeti za matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa fedha za ruzuku. Miongoni mwa mambo yaliyochangia kubadilika kwa ukomo wa bajeti ni kutenga fedha kwa ajili ya malipo ya posho za Waheshimiwa Madiwani pamoja na posho za mwezi kwa Watendaji wa kata

Baada ya mabadiliko yote yaliyofanywa kupitia vikao mbalimbali, kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri inategemea kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 52,636,564,958.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na nje. Mabadiliko haya yanatokana na kutolewa kwa ukomo mpya wa bajeti kwa mwaka huu wa fedha ambao ni zaidi ya uliotolewa mwaka 2020/2021.

